

JARIBIO LA TATHMINI LA PAMOJA LA 4MCK

CHETI CHA KUHITIMU MASOMO YA SEKONDARY KENYA (K.C.S.E.)

102/3

KISWAHILI

Karatasi Ya 3

JUNI – 2016

MUDA – 2 ½

Maagizo:

1. Jibu maswali manne pekee.
2. Swali la kwanza ni la lazima.
3. Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani:
Riwaya , Hadithi fupi, Fasihi simulizi na ushairi.
4. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
5. Kila swali lina alama 20.
6. Mtahiniwa ni lazima ahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawa na kuwa maswali yote yamo.

SEHEMU A: USHAIRI (alama 20)

1.(LAZIMA)

Mwanasiasa,

Mwanasiasa

Ni kijana aliyetumwa mafugani
Aliyewapeleka mifugo malishoni
Kisha akawa anafanya utani
Kupiga ukweli kuwaita insane
Kulalamikia mbwa mwitu asiyemwona machoni.

Mwanasiasa,

Ni mpanda ngazi tuliyetambiwa
Kuwa ngazi alipanda kwa kuchachawa
Kisha uko kileleni alipokuwa
Vichwa akawagota ngazi walomshikia

Mwanasiasa,

Umwonaye sana ukimuwarzia
Kisa cha zimwi utakumbukia
Lililoachwa na mama mjamzito kumpikia
Mhunzi alipoenda kazi kujichapia
Likageuka lafi kila kitu kukibugia
Mama, watoto, mbuzi, ng'ombe na hata mkia.

Mwanasiasa,

Wa bara hili ukitafuta yake mithili
Kinyonga ni yake tamthilikwa sifa ni riale kwa ya pili
Lakini ni mwendo wake ni wa haraka....

Mwanasiasa,

Nimwone
Nimujuaye
Nimsikiaye
Nashindwa kumwamini!

Maswali

- a)Eleza dhamira ya shairi hili? (al. 2)
- b)Kwa nini mtunzi anashidwa kumwamini mwanasiasa? (al.2)
- c)Onyesha namna mtunzi ametumia idhini yake ya utunzi huku ukitoa mifano wafaka? (al. 4)
- d)Bainisha **toni** ya shairi hili? (al. 2)

e)Jadili tamathali za usemi mbili alizotumia mwandishi kuwasilisha ujumbe wake? (al. 4)

f)Andika ubeti wa pili kwa lugha nadhari. (al.4)

g)Kwa kutoa ithibati , shairi hili ni aina gani? (al. 2)

SEHEMU YA B: TAMTHILIA: Mstahiki Meya – Timothy Arege.

Mstahiki Meya

2.Nanyi vile vile msikate tamaa. Endeleeni kushinikiza Meya. Mlango hatimaye huenda ukasalimu amri.”

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)

b)Huku ukitoa mifano, bainisha tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili. (al. 4)

c)Onyesha namna wanacheneo walivyojitalidi kuboresha hali zao. (al. 2)

AU

3.Eleza jinsi mbinu ya istiari ilivyotumika katika tamthilia ya mstahiki meya. (al. 20)

SEHEMU YA C: Riwaya. Ken Walibora.

KIDAGAA KIMEMWOZEA

4. “Ujenzi wa jamii mpya ni jukumu la vijana.” Jadili kwa kurejelea riwaya hii. (al. 20)

5.’Hata haramu huhalalishwa, ati, ‘Haramu ngapi zimehalalishwa? Chungu nzima.....’

a) Eleza muktasha wa dondoo hii. (al. 4)

b)Ni mbinu zipi za lugha zilizotumika katika kifungu hiki. (al 4)

c)Bainisha ukweli wa dondoo hili kwa kurejelea Riwaya nzima. (al. 12)

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

6.Mwanamke katika diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine amepewa nafasi finyu.

Fafanua kwa kuzingatia hadithi zozote nne. (al. 20)

AU

7.Tukio lililowaleta hapa ni la kawaida kwetu. Ingawa sisi hufanya tuwezayo kuwalinda wanetu, mara nyingi tabia zao hutupiga chenga.....

- a)Eleza muktadha wa dondo hili. (al. 4)
- b)Eleza sia nne za mzungumzaji. (al. 8)
- c)Jadili matatizo manne yanayojitokeza katika hadithi hii. (al. 8)
- SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**
- 8.i)Ngomezi ni nini? (al. 2)
- ii)Jadili changamoto za ngomezi ya kimapokeo katika jamii ya sasa. (al. 8)
- iii)Taja mifano miwili ya ngomezi za kisasa. (al. 2)
- iv)Fafanua hasara zozote nne za miviga katika jamii. (al. 8)